

# HUDUMA YA TAIFA IPONGEZWE

RAIS wetu Mpendwa Bwana Daniel Arap Moi, pamoja na serikali yake anastahili pongezi kwa uamuzi wake thabiti wa vijana kujiunga na Huduma ya Taifa baada ya kumaliza tu kidato cha sita ndipo waweze kujiunga na masomo mengine ya juu ama kuingia katika vyo Vikuu vya hapa nchini.

Raia wenye damu ya Nyayo wote waona kwamba hatua hii ni ya sawa iwapo kweli twataka kuwajenga vijana wetu waweze kuwa wananchi wenye dhamana siku za mbele.

Vijana wetu, mara tuwafikapo kidato cha sita huanza kunukiwa na harufu ya Utaalamu na kwa hivyo miondoko yake yote huwa ni ya kitaalamu. Pengine akipata likizo hawezi kufika mashambani akenda kuamkuwa babu na bibi yake kwani akitanya hivyo itabidi ajifanye kijana wa mashambani kwa kila jambo.

Yeye hawezi kufanya hivyo maana huwa ameshatoka katika hali hiyo ya maisha. Miji ambayo anaweza kuishi ni Nairobi, Mombasa labda na Nakuru.

Moja katika sababu za serikali kutaka kupeleka vijana katika Huduma ya Taifa, ni kutaka vijana wasome kwa vitendo. Yaani waende wakasome kwa kutumia mikono, maana kukaa darasani ukahubiriwa namna ya kujenga daraja haitoshi.

Baada ya kwisha pawa elimu ya sayansi ya daraja, linalofata ni kwenda kulijenga daraja lenyewe, kwa maana hapo utahakikisha kuwa vipimo vyako ni sawa ama si sawa, na hivi ndivyo vijana watakavyo wafanye. Mpaka lini nchi itajengewa madaraja na wataalamu kutoka nje ikiwa wataalamu tunalalanao nyumba moja?

Wale wasiopenda maendeleo, hivi sasa wapitikiwa ni kila mawazo ya kuishinda hatua hii ya serikali, lakini twaamini kwamba serikali iko macho. Baada ya jambo hili kupitishwa rasmi, hakuna mtu atakaye thubutu kucheza na serikali.

Kenya ina vijana wengi sana wenye nguvu nyingi sana na yataka nguvu zao zitumiwe kwa njia inayofaa ili ziweze kutoa mazao kwa faida ya nchi nzima. Badala vijana kukondomana katika miji ni kuharibu nguvu zao na maarifa yao bure ambapo mwisho humalizikia ulevi na ujangili.

Lakini kwa mpango huu, tuna tamaa vijana wetu watainua jina la Kenya.

**Aly Dagharoo,**
**MOMBASA.**

# WAISLAMU PWANI WAZIDISHE USHIRIKIANO

KWA muda wa siku nyingi Waislamu wa Pwani wameonekana ni watu ambao hawana maendeleo, na ijapokuwa Waislamu hawa hawa wa mapato ya kutosha kujiendeshea mambo yao lakini utaona bado wako nyuma isipokuwa kwenye mambo ya anasa za kipumbavu na zao kupoteza wakati.

Utaona makabila mengi ya Kihindi hapa Mombasa wako na shule za msingi na za upili lakini Waislamu hadi hivi leo hawana shule hata moja ya upili. Si hivyo tu ikiwa shule imepawa jina la Kiislamu au ina msingi wa Kiislamu, utaona mwisho wake huchukuliwa na makabila mengine kwa sababu wenyewe Waislamu wamezorota kimawazo.

*KIDOGO*

Tumeona mfano wa Khamis Secondary School ambapo katika shule hiyo wanafunzi kidogo tu ndio Waislamu. Na pia kuanzia mwakani lile somo la Dini ya Kiislamu, halitakuwa moja wa masomo ya mitihani.



*MSIKITI WA Shakombo kama ulivyo hivi sasa huko Mtongwe Vijiweni.*



*MCHORO WA Msikiti wa Shakombo kama utakavyo baada ya ujenzi mpya.*

## Wapenda kheri wajitolee

BWANA Hamisi Ramadhani Mwadzengo wa Sanduku la Posta 83100, Mombasa, Kenya, kwa aniaba ya watu wa Mtongwe Vijiweni, wanawatangazia Waislamu na wapenda kheri wote kwa jumla, ya kwamba wana Ujenzi wa Msikiti wa marehemu Shakombo Mwaurinda Jengo hili ambalo lilijengwa myaka 35 iliyopita, lataka kufanyiwa marakibisho na kujengwa upya ili upatikane msikiti wa watu kufanyia ibada bila ya wasi wasi.

Mipango ya Harambee ya jengo hili itatangazwa baadae, baada ya kwisha maliza mipango na kuzungumzwa na Wabunge na Madiwani wetu waliohusika.

Kila mwenye msaada wa aina yoyote, twamuomba amuandikie au amwite Mwandishi ambaye anuani yake ni hiyo hapo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye mlipaji hapa duniani na Kesho akhera.

Mfano wa pili ni Msikiti wa Miyome. Msikiti huu unafika thamani ya shillingi laki sita kuujenga. Na msikiti mzuri sana, lakini hivi sasa msikiti huo umegauzwa ghala ya kuwekea madawati mabovu. Jamani Waislamu wako wapi? Au wameshughulika na kusoma maulidi pekee?

Mtume Muhammad (S.A.W.) si alisema misikiti iimarishwe na isafishwe na itukuzwe? Sasa iwapo hatuifati hii amri ya Mtume wetu, baadae tujigamba kuwa twampenda Mtume. Kumpenda Mtume ni kupigana makumbo wake kwa waume katika zefe za Maulidi!

Napenda kutoa pongezi nyingi kwa wabunge wetu Sharif Nassir na Said Hemed, Meya wa Mombasa na wote wale ambao wamehusika na chuo cha Kiislamu ambacho kitajengwa Bamburi, kwa bidii yao waliyofanya hata wakaweze kupawa msaada wa fedha nyingi kutoka kwa Mwana wa Mfalme wa Abu Dhabi. Twaamini kwamba katika chuo hicho, Waislamu wa tapawa nafasi kubwa na haitakuwa mwisho kupigwa teke.

Pia nawapongeza Vijana wa Ujamaa kwa kazi yao kubwa ya kusimamisha jengo ambalo litakuwa na kazi mbali mbali, na pia watu wa Guraya kwa kujenga Madrasa kubwa ya kisasa.

Waislamu watakiwa wende mwendo huu na wajenge sio wabomoe.

**Zubeir Noor,**
**MOMBASA.**

# Ukimlea Mwana Mwema na mui naye mlee

**na SAID BURHAN**

**HAYO ndiyo mawaidha ya mmoja kati ya waimbaji wetu mashuhuri wa hapa Mvita ndugu Ali Mkali kwa jina hasa ni Ali Salim Anzuani.**

**Mara tu baada ya kuzaliwa mnamo mwaka 1936 katika mtaa wa Mwembe Tayari, alipawa jina hili la sare la Ali Mkali na bibi mmoja mtu mzima kwa vile alikuwa mlinzi sana. Ustadh Ali Mkali (kama waimbaji wote wanavyoitwa) alisoma katika Arab Boys School (Serani) na pia alikuwa akisoma dini katika Madrasatil Fallahi hapo Bondeni.**

**Ustadh Ali kama vijana wengi wa kiume alikuwa mcheza mpira mashuhuri. Timu yake ilikuwa Fallah Football Team. Timu hii aliwakilisha katika mikoa mbali mbali ya nchi ya Kenya. Mnamo mwaka wa 1935 wakati yeye ni kijana baro baro, alipendelea sana kuhudhuria hafla za arusi na sherehe nyenginezo.**

**Jambo lililokuwa likimvutia katika hafla hizo ni tarab. Wakati huo vyama vya tarab vya Johar na Morning Star vilikuwa vimetia fora katika mvita na pia Mwambao wa Afrika Mashariki. Ustadh Ali asema kwamba yeye binafsi alivutiwa na uimbaji wa waimbaji kama vile Nassor Wachaka na Athman Muhalla ambao wote walikuwa waimbaji wa Johar.**

**Mwanzo wa kuimba kwake, alianza na chama cha Star, kisha akajiunga na chama cha Johar. Baada ya chama cha Johar, alijiunga na Lulu, na baada ya hapo aliunda okestra yake mwenyewe aliyoiita Mvita Okestra.**

**Na ni katika chama hichi chake ndipo alipo komaa kama muimbaji. Katika nyimbo zake za asili ambazo zilipendwa sana na pia zikatia fora katika Sauti ya Mvita ni kama hizi: Bembeya mtoto, Wacha waseme, Mtungi umevunjika, Howa howa mtoto, Shilingi yang'ara yaua, Alby, Ukilea mwana mwema, Mafundi pamba na kadhalika.**

**Na jambo la ajabu kuhusiana na uimbaji wa Ustadh Ali, ni kwamba mashairi ya nyimbo zake huyatunga yeye mwenyewe. Na yeye apendelea zaidi utunzi wa maisha ya kibinadamu au wasia.**



*• ALI MKALI*

**Ustadh Ali aliwacha kuimba myaka mingi sasa. Sababu ya yeye kuacha kuimba, anasema ni kufungwa kwa Sauti ya Mvita. Na iwapo leo tu idhaa hiyo yafunguliwa tena basi yeye ataanza kuimba upya na pia wale waimbaji mashuhuri kama Miraji Juma aliyeimba "Muhogo" wanaweza wakajitokeza tena na kusikika hewani.**

**Yeye fikra zake ni kwamba utamaduni na lugha ya Kimvita hupatikana katika nyimbo zake. Waimbaji wengine wa Kimvita huigiza mahadhi ama sauti ya Kihindi na hivyo nyimbo zao japokuwa ni nzuri masikioni lakini kiutamaduni hazina umuhimu.**

*IMARA*

**Ustadh Ali anasema sauti yake hadi hivi leo ni imara kabisa kwani huifanyia mazoezi mara kwa mara. Na hamu yake sana sasa ni kuona kwamba nyimbo zake zanaswa kwa kanda za sauti na kuhifadhiwa katika majumba ya ukumbusho kwa wale watalii ambao hufika hapa nchini kwa minajili ya kutafuta utamaduni wetu.**

**Pia anahimiza wapenzi wa nyimbo zake wafanye mpango hata ikiwa ni wa harambee ili aweze kujenga tena okestra yake kwa faida ya wakaazi wa Mvita. Na yeye hata hivi sasa yuko tayari kuimba kwenye hafla za harusi kama vikundi vyengine. Kina mama mnakaribishwa.**

# TWAWATAKIA WASOMAJI KRISMASI YA HERI

SHEREHE ZA Siku Kuu ya Krismasi zimewadia na Wakenya kote nchini wamejiandaa kwa sherehe hizo kwa kununua vifaa mbali mbali pamoja na tikiti za kusafiria ili kujumuika pamoja na jamaa zao sehemu za bara ama kwengineko. Tukiwa kama gazeti, hatuna budi kuwatakia raia wa nchi hii Krismasi ya heri yenye furaha. Pia wasomaji wetu popote pale walipo twawatakia Krismasi yenye furaha.

Hapa Pwani, tulizoea kuwa pamoja Rais wetu kila Siku Kuu ya Krismasi tangu ifikapo tokeauhai wa marehemu Mzee Jomo Kenyatta. Rais Moi alianza kufata mpango huu, yaani kuja Pwani kwa mapumziko mafupi wakati wa Krismasi. Lakini mara hii, Rais wetu mpendwa hakuwahi ama hatawahi kuja Pwani kwa ajili ya kazi nyingi za kiserikali. Kwa hivyo huko huko aliko, twamtakia Rais wetu pamoja na watoto wake Krismasi ya furaha na amani na vile vile twamuombea baraka za mwaka mpya. Mungu ampe nguvu na afya ili mwaka wa 1981 ukingia atuongoze kwa bidii zaidi na atupeleke kwenye mafanikio.

Katika muda huu wa kusherehekea Krismasi, Wakenya wataka wajiepushe na kila jambo ambalo lingedhuru watu wengine kwani sherehe humalizika kwa furaha hazimaliziki kwa misiba. Watu wa kwanza ambao twapenda kuwaasa kwa manzili haya ni madereva. Wakati wa Krismasi, huwa kuna misafara miretu ya magari baina ya Nairobi na Mombasa. Jamaa wengi kutoka Bara huja Pwani kwa Krismasi. Na baadhi ya hawa huendelea mpaka Malindi na Lamu. Twawaomba madereva wapeleke magari kwa uangalifu zaidi. Misiba ya vifo wakati wa sherehe huumiza sana. Toka kuzuiwa magari makubwa ya mizigo kusafiri usiku, ajali zimepungua.

Ununuzi wa bidhaa ni budi ufanyike kwa kufikiriana ili kila mmoja aweze kupata. Kwa mfano, mtu mwenye nafasi ya pesa iwapo atakwenda dukani anunue marobota mane matano ya unga, atazuilia wenye nafasi ndogo ya matumizi kupata hata riziki ya kupika siku moja na watoto wake. Vipi utashiba na jirani yako alale na njaa wakati wa Siku Kuu?

Majambazi ni kundi jengine la watu la kuonywa na kuchunguzwa vizuri na walinda usalama humu nchini. Hakuna mwenye mawazo ya kurudi kazina baada ya Krismasi akakuta nyumba yake imevunjwa ama duka lake limevunjwa. Wananchi wanahitaji ulinzi kamili ili wakati wanaposherehekea wasiwe na wasi wasi katika roho zao.

Wafanyi biashara katika kundi la wanyonyaji wataka wamulikwe sana. Hawa wana vitimbi vikubwa sana ifikapo Siku Kuu ya aina yoyote. Kwa vile wao huona kwamba raia lazima watahitajia bidhaa kwa ajili ya sherehe na karamu zao, wao huanza kubadilisha bei za bidhaa mnamo masaa ya usiku. Raia wakirauka asubuhi bei ni nyengine. Raia wakiwa katika harara ya kununua huwa hawajali kupeleleza magauzi haya ya bei kwa hivyo hupoteza pesa nyingi sana. Maafisa wetu waliohusika na bei za bidhaa madukani mwa reja reja yataka wachukue hatua ya ili wawanusuru raia wasiibiwe na wafanyi biashara wapendao uta jiri wa haraka haraka.

Twauombea mwaka wa 1981 uwe mwaka wa mafanikio na amani katika nchi ya Kenya.

# COASTWEEK ★ ★ ★ ★ KARAMSHI HARJI

**SHARP EL-211**
**Electronic Calculator**
Coast Agents:
**KARAMSHI HARJI**
Box 81777 Tel: 312575
MOMBASA



## SWAHILI CROSSWORD NO. 107



*KWENDA KULIA:*

1. Mto wa Zambia
5. Kiungo cha kukataa
6. Kuwa baridi
7. Aina ya embe
8. Ama
10. Rafiki
11. Juhudi, ghera
12. United Kingdom
14. Teketeza
16. Si P.M.
17. Medical Officer

*KWENDA CHINI:*

1. Sumbua, babaisha
2. Ni mdudu kisha ni nguo
3. Zaidi
4. Kiungo cha maneno
5. Kivazi cha kike
9. Wa kutukiza
12. Uza imepungua
13. Ngapi?
15. Ala, jalada

**JINA.............................................**

**SANDUKU LA POSTA..............................**

.............................................

### Mshindi wa Fumbo la Kujaza Maneno No. 106

S. Ali Attwas, Sanduku la Posta 80306, Mombasa.

Mshindi aombwa afike afisini mwa *COASTWEEK*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 106 —**

*KWENDA KULIA:*

1. MAKUBADHI, 6. UIMBAJI, 7. MEA, 8. DHIHAKA, 11. YA, 12. NINGA, 13. MAWE, 14. HASAMA.

*KWENDA CHINI:*

1. MUUNDI, 2. KAMBI, 3. BWANA, 4. DAIMA, 5. ISHARA, 9. HONGA, 10. KWAMA, 11. YOWE, 12. NOA

### Shindano la Fumbo la Kujaza Maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Mshindi wa kwanza kila baada ya wiki mbili atapata zawadi ya Sharp EL-211 Electronic Calculator. Shindano hili limedhaminiwa na *COASTWEEK LTD* pamoja na KARAMSHI HARJI Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri, *COASTWEEK*, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya. Siku ya Jumatano tarehe 31.12.80 saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.